# Hali ya mifumo ya takwimu za watoto wanaozaliwa wakiwa wamefariki (stillbirths) barani Afrika

## MUHTASARI


**Utangulizi:**
Vifo vya watoto vinavyotokea wakati bado wakiwa tumboni mwa mama mjamzito (stillbirth) vimeendelea kuwa tatizo kubwa lisilopewa kipaumbele katika afya ya jamii ambapo takribani watoto milioni 1.9 huzaliwa wakiwa wamefariki kila mwaka duniani — wengi wao wakiwa katika nchi za kipato cha chini na cha kati.. Licha ya ukubwa wa tatizo hili, ukusanyaji, uainishaji, na matumizi ya takwimu za vifo hivyo zinatofautiana sana baina ya nchi, jambo linalopelekea mwitikio hafifu katika juhudi za kukabiliana nalo ipasavyo. Kwa kushirikiana na **Africa CDC** na **UNICEF, Chuo Kikuu cha Cape Town** kilifanya utafiti katika nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kutathmini hali ya mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za vifo hivyo, ikiwemo tafsiri zinazotumika kuanisha watoto wanaozaliwa wakiwa wamefariki, sera, uchakataji na matumizi ya takwimu hizo.

**Mbinu za utafiti:**

Utafiti wa mtandaoni (*cross-sectional online survey)* ulifanywa kati ya mwaka 2022 na 2023, ukihusisha wadau wanaoshughulikia afya ya mama na mtoto mchanga kutoka nchi zote 55 za Umoja wa Afrika. Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna vifo vya watoto kabla ya kuzaliwa vinatafsiriwa, mifumo ya sera, mbinu za ukusanyaji wa takwimu za vifo hivi, na njia zinazotumika katika matumizi ya hizo takwimu. Majibu ya tafiti yalihakikiwa kupitia ufuatiliaji wa taarifa katika nchi husika ikiwemo mapitio ya taarifa fupi zinazoielzea nchi na warsha za mrejesho wa kikanda. Takwimu zilichakatwa na taarifa iliandaliwa.

**Matokeo:** Kati ya nchi 55 zilizoalikwa kushiriki utafiti huu, nchi 33 ziliwasilisha majibu na nchi 30 zilikamilisha utafiti kama ilivyotakiwa. Matokeo yalihusisha;

- **Tafsiri:** Namna vifo hivi hutafsiriwa zilitofautiana; tafsiri iliyotumika maeneo mengi zaidi ilikuwa ni kifo kinachotokea wakati mimba ina umri wa wiki 28 na zaidi au wakati mtoto (akiwa tumboni) amefikisha uzito wa gramu 1000.
- **Sera:** Nusu ya nchi zilizohusishwa katika tafiti zimejumuisha aina hii ya vifo katika mifumo ya kisheria, ingawa baadhi hazina sera kuhusu uainishaji, mapitio, na uwekaji malengo.
- **Matumizi ya takwimu**: Takribani nchi zote ziliarifu kwamba taarifa za aina hii ya vifo huchukuliwa kama taarifa zikusanyazwo kila siku kupitia sekta ya afya kwa kutumia karatasi maalumu na huainishwa kwa kutumia tafsiri iliyoafikiwa kitaifa. Ukusanyaji wa takwimu hizi hutofautiana baina ya nchi, ambapo nchi nyingi hutegemea takwimu kukusanywa kutoka vituo vya afya kwenda kwenye mifumo ya kitaifa. Asilimia 79 ya nchi (nchi 26 kati ya 33) ziliarifu kutumia mfumo sanifu wa uainishaji wa visababishi vya vifo hivi, ambazo mara nyingi hufanyika katika ngazi ya vituo vya afya kupitia madaktari na madkatari ngazi ya diploma, ingawa utaratibu na kada zinazotumiwa kuanisha sababu za vifo hutofautiana. Changamoto katika kukusanya na kuwasilisha takwimu katika ngazi za vituo vya afya na kitaifa ni pamoja na uchache wa rasilimali kwa ajili ya mifumo inayokusanya taarifa sza kila siku na rasilimali za huduma za afya ya mama na mtoto mchanga. Changamoto nyingine ni pamoja na uwezo mdogo wa watumishi katika kukusanya na kutumia takwimu.
- **Matumizi na usambazaji wa takwimu:** Zaidi ya asilimia 60 ya nchi zina kamati katika ngazi mbalimbali za kupitia takwimu ya vifo hivyo, lakini matumizi yake hukwamishwa na ukosefu wa rasilimali na uwezo. Nchi

21 (64%) hutayarisha ripoti za kitaifa zenye data za aina hii ya vifo kwa wizara za afya, ingawa 17 pekee (52%) ziliarifu kuzichapisha hadharani.

**Hitimisho na mapendekezo:**

Taarifa hii inatoa picha ya sasa ya mifumo ya takwimu za vifo vya watoto vinavyotokea kabla mtoto hajazaliwa barani Afrika kwa mwaka 2023–2024. Nchi zinaweza kuwekwa katika makundi matatu ya utayari: (1) zile zenye mifumo iliyopo inayohitaji kuimarishwa; (2) zile zenye sera zisizijitosheleza au zenye utekelezaji hafifu wa sera na (3) zile zinazohitaji msaada katika kuijenga mifumo. Ili kuboresha ufuatiliaji na matumizi ya takwimu hizi, kunahitajika uwekezaji katika sera za kitaifa, uunganishwaji wa mifumo ya takwimu, na katika kuwajengea uwezo wafanyakazi. Mwongozo wa kikanda, tafiti za utekelezaji, na uainishaji wa mifano bora (case studies) vinaweza kusaidia nchi kukusanya na kuzitumia takwimu.

Access the report: https://africacdc.org/improving-stillbirth-data-recording-collection-and-reporting-in-africa/

Report to be launched on 25 October 2025 at the Conference of Public Health in Africa